# HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

# TANGAZO

## YAH: **MAELEKEZO KUHUSU UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA UTAKAOFANYIKA TAREHE 24 NOVEMBA, 2019**

1. **UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA**
   i. Zoezi la Uandikishaji na Uandaaji wa Orodha ya Wapiga Kura litafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa kuanzia tarehe **8/10/2019** hadi tarehe **14/10/2019**.

   ii. Vituo vya uandikishaji wa wapiga kura **vitafunguliwa kuanzia saa mbili kamili asubuhi** na **kufungwa saa kumi na mbili kamili jioni.**

   iii. Mkazi yeyote mwenye umri wa kuanzia **miaka kumi na nane (18) na kuendelea** anatakiwa kujitokeza kujiandikisha kwenye orodha ya wapiga kura katika Mtaa anaoishi.

iv. Chama cha Siasa kitaruhusiwa kuteua wakala wake kwa kila kituo cha uandikishaji wa wapiga kura wakati wa uandikiashaji wapiga kura kwa gharama za chama husika.

v. Mkazi ambaye amejiandikisha katika Orodha ya wapiga Kura atakuwa na haki ya kukagua orodha ya wapiga kura kwa muda wa siku saba kuanzia tarehe **15/10/2019** hadi tarehe **21/10/2019** ambayo itabandikwa katika sehemu ya matangazo ya uchaguzi ili;

   a) Kuweka pingamizi kuhusu usahihi wa orodha hiyo;
   b) Kuomba Orodha irekebishwe kwa;
      - Kuongeza jina lake;
      - Kubadilisha taarifa zilizoko katika orodha hiyo; au
      - Kufuta jina lililoorodheshwa kwa vile aliyeorodheshwa amefariki.

vi. Pingamizi dhidi ya orodha ya wapiga kura litawasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Mtaa ambaye atatoa maamuzi dhidi ya pingamizi hilo.

vii. Endapo mtu aliyeweka pingamizi au aliyewekewa pingamizi hatoridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuhusu pingamizi lilowasilishwa kwake, mtu huyo atawasilisha Rufaa kwa Msimamizi wa Uchaguzi kuanzia tarehe **21/10/2019** mpaka **23/10/2019**. **Aidha uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu Rufaa iliyowasilishwa kwake utakuwa wa mwisho.**

2. **SIFA ZA WAGOMBEA**

Mkazi yeyote wa Mtaa atakuwa na haki ya kugombea uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa endapo;

a) ni raia wa Tanzania;
b) ana umri wa miaka **ishirini na moja (21) au Zaidi;**
c) ana uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza;
d) ana shughuli halali ya kumwezesha kuishi;
e) ni mkazi wa eneo la Mtaa;
f) ni mwanachama wa Chama cha Siasa na amedhaminiwa na Chama hicho;
g) hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi; na
h) hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

3. **UTEUZI WA WAGOMBEA**

i. Uteuzi wa Wagombea wa Uchaguzi utafanyika tarehe **05 Novemba, 2019** na Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi.
ii. Majina ya Wagombea yatabandikwa katika mbao za matangazo zilizopo kwenye Ofisi za Serikali za Mitaa za Mitaa husika.
iii. Kuanzia tarehe **05 Novemba, 2019** hadi tarehe **06 Novemba, 2019** mtu yeyote aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea au mgombea yeyote anaruhusiwa kuwasilisha **Pingamizi la Maandishi** kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi dhidi ya uteuzi wa mgombea.
iv. Msimamaizi Msaidizi wa Uchaguzi atasikiliza na kutoa uamuzi dhidi Pingamizi lililowasilishwa kuanzia tarehe **05/11/2019** hadi tarehe **07/11/2019**.

v. Mwombaji au mgombea ambaye hataridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kukata Rufaa kwenye **Kamati ya Rufaa kuanzia tarehe 05/11/2019 hadi tarehe 08/11/2019.**

vi. Kamati ya Rufaa itapokea, itasikiliza na kutoa uamuzi dhidi ya Rufaa iliyowasilishwa na Mwombaji au mgombea kuanzia tarehe **05/11/2019** hadi tarehe **09/11/2019**. Aidha uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

vii. Mtu aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea au mgombea ambaye hataridhika na uamuzi wa kamati ya Rufaa atakuwa na haki ya kufungua shauri katika Mahakama ya Wilaya ndani ya muda wa **siku thelathini baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa.**

4. **KAMPENI ZA UCHAGUZI**

i. Kampeni za uchaguzi zitaanza tarehe **17 Novemba 2019** hadi tarehe **23 Novemba 2019.**

ii. Mikutano ya Kampeni za uchaguzi **itaanza saa mbili kamili asubuhi** na **itamalizika saa kumi na mbili kamili jioni** ya kila siku ya kampeni.

iii. Mgombea au mwakilishi wa mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea hakitaruhusiwa kuendesha kampeni za uchaguzi kwa;

a) kutumia rushwa;
b) kutoa maneno ya kashfa au lugha za matusi;
c) kufanya ubaguzi wa jinsia, maumbile, ulemavu, dini, rangi, kabila au ubaguzi mwingine wa aina yoyote; au
d) kutoa maneno ambayo yanaweza kusababisha uvunjifu wa amani au kusababisha vurugu.

5. **UKOMO WA VIONGOZI KUWA MADARAKANI**

   i. Viongozi wote wa Serikali za Mitaa **watakoma kushika nafasi za uongozi tarehe 22/10/2019.**

6. **UCHAGUZI**

   i. Uchaguzi utafanyika tarehe **24 November, 2019.**

   ii. Uchaguzi utafanyika kwenye vituo vya uchaguzi walikojiandikisha wapiga kura.

   iii. Kura zitapigwa kuanzia saa **mbili kamili asubuhi** mpaka **saa kumi kamili jioni.**

   iv. Mkazi yeyote wa Mtaa atakuwa na haki ya kupiga kura endapo atakuwa na sifa zifuatazo**;**
      - ni raia wa Tanzania;
      - ana umri wa miaka kumi na nane (18) au zaidi;
      - ni mkazi wa eneo la Mtaa husika;
      - hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu; na
      - awe amejiandikisha kupiga kura katika Mtaa anoishi.

   v. Mtu hatakuwa na haki ya kupiga kura endapo;
      - hana mojawapo ya sifa zilizoanishwa katika aya namba **iv** hapo juu; au

- amejiandikisha kupiga kura katika kituo zaidi ya kimoja.

vi. Siku ya kupiga kura, mpiga kura atatakiwa kuonesha mojawapo ya vitambulisho vifuatvyo;
   - Kitambulisho cha mpiga kura;
   - Kitambulisho cha kazi;
   - Hati ya kusafiria;
   - Kadi ya Bima ya Afya;
   - Kitambulisho cha Shule au Chuo;
   - Kitambulisho cha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;
   - Leseni ya Udereva; au
   - Kitambulisho cha Taifa.

vii. **Mtu yeyote hataruhusiwa kubaki katika eneo la kituo cha kupigia kura baada ya kupiga kura.**

***Kwa Tangazo hili, wananchi wote mnaombwa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kupiga kura, kugombea na kushiriki katika uchaguzi huu ili kupata viongozi bora wa Serikali za Mitaa kwa maendeleo ya nchi yetu.***

Limetolewa tarehe 23/09/2019

**ROSEMARY J. MSASI**
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**
**KIBAHA MJI.**